# Rushwa na kizungumkuti cha uwajibikaji pasipo na utashi wa kisiasa

Na Beda Msimbe

RUSHWA bado ni tatizo la Watanzania wengi hasa wale wachumia juani kutokana na athari zake katika juhudi zao za kutengeneza maisha.

Kama vile rushwa ni sehemu ya maisha ya Watanzania imekuwa na utata mkubwa wa kupewa tafsiri na maana kiasi cha kupoteza mwelekeo sahihi wa kukabiliana nayo.

Kwa wale wanaofuatilia majibizano katika majukwaa ya kisiasa atamaizi kuwa rushwa na makandokando yake bado ni shida kubwa kwa Watanzania, ndio maana ikapata majina kama 'takrima', 'cha juu', 'mlungula' na mengi mengineyo.

Katika majadiliano ya wafanyabiashara wa sekta binafsi na umma yaliyofanyika mwishoni mwa wiki, rushwa ilitawala na ikatolewa maelezo kadhaa yenye kuleta utata.

Bila kutaja hotuba ya Rais Jakaya Kikwete muda mfupi baada ya kupata Urais, kiongozi huyo alionesha utashi wa wazi wa kisiasa wa kukabiliana na rushwa, akizungumza hoja za wananchi, za viongozi wao kutopea katika utajiri usiokuwa na maelezo.

Alisema vijijini unaona mtu aliyekonda na ng'ombe aliyekonda, lakini kwa upande mwingine unaona mtu anayeibuka katika utajiribaada ya kupata madaraka bila kuwapo kwa maelezo yanayokidhi akili kapataje utajiri huo katika muda mfupi.

Aidha vikumbo vya kuwania uongozi vinashinikiza matumizi makubwa ya fedha na japokuwa ziliundwa taasisi za kushughulikia rushwa bado utaratibu wa mahakama za Tanzania zimefanya wanaokamatwa wakiwa wachache, tena wala rushwa wadogo wadogo, huku maisha yakiwa na kero na manung'uniko ya kutotendewa haki.

Wanaotafuta nafasi za kisiasa walio na fedha wengi ni wafanyabiashara wakijua kwa nini wanataka kufanya siasa lakini kauli za wafanyabiashara katika mkutano wa majadiliano kati ya sekta ya umma na watu binafsi wameonesha uwanja mpana zaidi wa rushwa.

Huku Tanzania ikidaiwa kuwa miongoni mwa mataifa 14 yanayotopea kwa rushwa, mmoja wa wafanyabiashara, Dk Reginald Mengi aliyepewa nafasi ya kuzungumza alisema sentensi mbili za mwanzo ambazo zilikuwa na maswali zaidi kuliko majibu.

Rosemary Mwakitwange mmoja wa waendesha mjadala huo alimchokoza Dk Mengi kueleza kama mmoja wa wafanyabiashara wakubwa na huenda kama mmoja ayemiliki nyumba kubwa ya habari nchini (IPP MEDIA GROUP) analionaje shindano la katuni kuelezea mazingira ya ufanyajibiashara nchini limetawaliwa na katuni za rushwa.

Mengi hakutaka kuzungumza neno lakini alipobanwa tena alisema: "Kutoka katika Biblia unaona mstari ulioandikwa wana masikio lakini hawasikii, huku kwenye Kurani Tukufu kuna 'wana masikio, wanasikia lakini hawaelewi."

Kimsingi katika majadiliano hayo ya mwishoni mwa wiki ilionekana dhahiri kwamba hakuna mtu ambaye anataka kwenda moja kwa moja na hata maneno ya mmoja wa wafanyabiashara wanaoeleza kukerwa na kuathiriwa na rushwa (Dk Mengi) bado huoni maelezo ya kuridhisha yaliyo wazi.

Katika majadiliano hayo ya wafanyabiashara wakati wa uzinduzi wa taarifa hiyo iliyofanyiwa utafiti na Sekta Binafsi kwa ufadhili BEST AC, Programu iliyopo ofisi ya Waziri Mkuu, ilionekana wazi kwamba kuna utashi wa kisiasa lakini hakuna uwajibikaji.

Pamoja na rushwa kuonekana kuwapo kwenye ujasiriamali kwa madai kuwa wenye uwezo sasa wanakamua msuli katika mambo mengi ili waweze kufanikisha mambo yao mifumo ya kodi nchini inasababisha rushwa kutokana na ukweli kuwa, wafanyabiashara wamewekewa mzigo mzito wasioweza kuutua kirahisi.

Watu wanaosindika maziwa walisema wana sheria 25 za kuzingatia, wana taasisi 15 za kuwadhibiti na gharama ya kutii sheria hiyo kabla ya kuanza kazi ni shilingi milioni 12.

Walisema katika mazungumzo kwamba inachukua miezi sita kukamilisha usajili na mwaka unaofuata wanatakiwa kuwa na shilingi milioni 48 ili waweze kutii sheria ya leseni na uendeshaji wa usindikaji maziwa.

"Mlolongo mzima unafungua milango ya rushwa," alisema mwakilishi wa viwanda vya usindikaji maziwa nchini na kuhoji kwa nini vitu vyote visilipwe kwa mkupuo mmoja na eneo moja na badala yake mtu anahangaika kutoka kijijini, Serikali ya Mitaa, Serikali Kuu na mamlaka za usimamizi wa kanuni?

Mfanyabiashara aliyejitambulisha kwa jina la Tatu ambaye anasema yeye ananunua korosho na kusindika alizeti anasema mlolongo wa kupata vibali na leseni umegubikwa na tozo kibao, tozo ambazo zinaonekana wazi kushawishi rushwa.

Mtu wa Vibindo, Gasgton Kikui, anasema mifumo ya ulipaji wa kodi ni chanzo cha rushwa ambayo si tu inatia upofu lakini pia inasababisha uwekezaji nchini Tanzania, hasa kwa wachumia juani kuwa tatizo kubwa.

Yeye anasema kwamba uhusiano wa maofisa wa Mamlaka ya Mapato na wajasiriamali wadogo ni wa paka na panya, wa vijijini akisema kwamba wale wa mjini hawawindwi hata siku moja kwa hiyo hawana mashaka.

Sentensi yake hiyo ina maana kubwa zaidi ikichambuliwa kiupekee lakini alisema wazi kwamba kodi zilizopo zinatoa mwanya mkubwa wa rushwa na ukwepaji kwa kuwa maofisa wa Mamlaka ya Mapato huko vijijini wanatazama wajihi wa mtu kutoza kodi na wala si ripoti walizonazo za biashara inayofanyika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini Tanzania (TPSF) Godfrey Simbeye wakati akizindua kitabu cha 'Mitazamo ya Viongozi wa Biashara Juu ya Mazingira ya Uwekezaji Tanzania' anasema kwamba wakati umefika kwa Serikali kuweka kipaumbele katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kuikabili rushwa inavyostahili.

Kauli yake hiyo ilifanana na ya Dk Mengi wakati alipopata nafasi nyingine ya kuzungumza ambapo alisema kwamba kwa kukabiliana na wala rushwa wakubwa wanaoyumbisha nchi, Taifa linaweza kuondokana na aibu ya kuitwa taifa la rushwa na pia kukomesha mlipuko wa biashara ya dawa za kulevya.

Dk Mengi alisema ana uhakika kwamba fedha za rushwa hutumika kuimarisha uingizaji wa mihadarati nchini au kuitoa na hata kukamatwa kwa wasichana wawili wasanii wa Kitanzania nchini Afrika Kusini wakiwa na dawa za kulevya zenye thamani ya Sh bilioni 6.8 kunaonesha nini kinaendelea nchini.

Bila kutaja majina yao alisema mabinti hao hawana uwezo wa kupata fedha za kununulia mzigo wa thamani hiyo na kusema kwamba kazi hiyo inawezeshwa na watoa rushwa wakubwa nchini ambao wanajulikana.

Wasanii waliokamatwa hivi karibuni na mzigo wa dawa za kulevya nchini Afrika Kusini ni Agness Gerald 'Masogange' na Melis Edward.

Kwa maneno yake mtu unaweza kutafsiri kuwa taifa hili linasumbuliwa na watoa rushwa wanne wakubwa ambao wamefanya hata uwekezaji kugubikwa na matatizo yanayotokana na harufu yao.

Dk Mengi anasema tatizo hilo kubwa la rushwa kwa taifa kwa sasa linaweza kuondoka kama hatua za kijasiri za kuwakataa watu hao zitachukuliwa na wala isiwe kuwepo kwa utashi wa kisiasa pekee wakati uwajibikaji haupo.

"Taifa likubali kutengana na watoa rushwa wakubwa haraka na mara moja na taifa litaendelea kuishi," anasema Dk Mengi.

Dk Mengi katika ufafanuzi zaidi wa ukubwa na tatizo la rushwa anakiri kwamba yeye ni mmojawapo wa watu wa Tanzania walioumia katika rushwa kwani amepoteza miradi miwili mikubwa kutokana na rushwa.


Kibwagizo kwamba Watanzania wenyewe hawapendani na kukaripia matukio ya rushwa na kutoa mfano kwamba yeye (Dk Mengi) alipolalamika kuhusu Hoteli ya Kilimanjaro, yupo mtu aliyeuliza kwa nini Mengi anataka kushika kila kitu kinaweza kutafsiri kwa namna nyingi zaidi na kuonesha kwamba rushwa inaumiza kila mtu.

Mashaka kwamba Serikali haisikilizi kilio cha wafanyabiashara pia kinafanya hata juhudi za kusema zisiwepo.

Watu wa Ethiopia waliokuja kujifunza athari za rushwa Tanzania walipoulizwa na wenzao wa sekta binafsi nchini hali ikoje walisema kwamba rushwa inakabiliwa kwa nguvu zote na mikoa mingi ina watuhumiwa waliofikishwa mahakamani na waliochukuliwa hatua.

Naye Mtendaji wa Sekta Binafsi, Godfrey Simbeye alisema Waethiopia walishangazwa kusikia

Inaendelea Uk 24



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), Godfrey Simbeye akizungumza katika majadiliano ya wadau wa sekta binafsi.



Dk Reginald Mengi akiwa na Hans Determeyer, Meneja mradi wa Best Ac ulioratibu mazungumzo ya wadau sekta binafsi.